BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 15 Mei, 2025**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

43. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, ulipitishwa mwaka 1985 na kuridhiwa na Tanzania mwaka 1996 ikiwa ni miongoni mwa nchi 10 zilizizopo kwenye ukanda huu.

Ripoti za utekelezaji wa mkataba huu zinaitaja Zanzibar kama sehemu ya Tanzania katika kutekeleza mkataba huu wa kuhifadhi mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Zanzibar imeshirikishwa katika utekelezaji wa mkataba huu muhimu.

(b) Je, ni miradi mingapi Zanzibar imewahi kufaidika kupitia mkataba huu tokea kuridhiwa Tanzania.

(c) Kwa kuwa mikataba hii hutekelezwa kwa nchi wananchama kuchangia michango katika mfuko mkuu, ni kiasi gani Zanzibar hutakiwa kuchangia.

**Ofisi ya Rais - Ikulu:**

188. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Ikulu:

Ni mageuzi gani ya msingi ya kujivunia kwa ndugu zetu wa Diaspora.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Wajasiriamali wengi wanapata changamoto ya kukabiliana na ongezeko la matumizi ya teknolojia katika kuzalisha na kusambaza bidhaa na huduma za kifedha.

Kwa kiasi gani Serikali inawasaidia wajasiriamali hawa ili waweze kutimiza ndoto zao ipasavyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

243. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Usafiri wa boda boda umerahisisha safari katika visiwa vyetu ambapo asilimia 80 ya madereva wake ni vijana. Hata hivyo, baadhi ya vijana wanaendesha vyombo hivyo bila ya kuwa na leseni kwa madai kwamba upatikanaji wake unakuwa na usumbufu.

(a) Ni lini huduma ya leseni itatolewa katika Wilaya (Halmashauri au Mabaraza ya Mji) badala ya kuwa Mjini pekee (Makao Makuu).

(b) Kwa kuwa hivi sasa waendesha boda boda wamekuwa kero kwa jamii. Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wake.

(c) Ni zipi hatua zinazochukuliwa ili kuondosha kero za boda boda kwa jamii.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

271. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tuna miradi ya maendeleo mingapi kwa sasa kupitia sekta ya kilimo na ina udhamini kutoka mataifa yepi ya kigeni.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

68. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuna maeneo mengi yanayotambulika kihistoria na kuwekewa kumbukumbu yakiwemo makaburi ya watu ambao walifika hapa Zanzibar.

Ni maeneo gani ambayo yamefanyiwa tafiti hizo na kujua historia zao.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2025/2026.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BAR.AZA**

**Zanzibar,**
**15 Mei, 2025.**